# POST MOCK TEERM 3 2019

## *Kenya Certificate of Secondary Education (KCSE)*
## *September 2019*

102/2
**KISWAHILI**
KARATASI YA PILI

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA KISWAHILI

---

**UFAHAMU**

**1.** - Mtoto anaweza kukosa huduma za kimsingi
- Watoto hukosa mwelekeo

2x1=Alama 2

2. Tofauti kati ya wazazi/wazazi kutoelewana katika ndoa 1x1 = Alama 1

3. – Utamaduni huwezesha jamii kuyaona mambo kwa mtazamo mmoja.
- Hutuwezesha kuwa na umoja
- Hututambulisha Kama jamii
- Hukuza maadili miongoni mwa wanajamii

Zozote 2x1 = Alama 2

4 - Kwa sababu ya hali ya ngumu ya maisha inayowafanya watu kupata watoto wachache wanaoweza kumudu kuwalea
- Kupungua kwa nafasi za ajira huwazuia vijana kuingia kwa nikahi mapema.

2x1 = Alama 2

5. Misemo – kuingia katika nikahi →kuolewa
Methali – samaki hukunjwa akiwa bado mbichi
Tashhisi – kitengo cha familia kimesakamwa na wimbi kali la mabadiliko

3x1 = Alama 2

6 (a) Kimesakamwa – kimesongwa / kimekabiliwa sana.
(b) Mfarakano usiokwisha – ugomvi usio na kikomo
(c) Wahalifu waliokubuhu – wahalifu / watenda maovu waliobobea / waliozoea
(d) Vikoa vimekwisha – utangamano / ujamaa umekwisha
(e) Kujivika mavazi mawili – Kuwa na tabia aina mbili – nzuri na mbovu

5x1 = Alama 5.

**II UFUPISHO**

(a) - Makundi ya watu wanaohasimiana ndio chanzo cha ugaidi.
-Nia huwa ni kulipiza kisasi kwa vile kundi moja hujihisi kuwa dhaifu.
- Kiini cha uhasama huwa dini, uchumi au siasa
- Mashambulizi haya huwa na athari nyingi k.v.
-Watu kuuawa
-Ulemavu
-Kuvuruga maisha ya watu
-Elimu huvurugwa
-Matatizo ya kisaikologia
-Kuharibu mali
-Usalama wa nchi huwa mashakani
-Utalii huathiriwa

Hoja zozote 9 x1 = 9

Utiririko 1x1 = Alama 1

(b) Njia zinazotumiwa kupambana na ugaidi
-Kutumia mtutu wa bunduki / kushambulia magaidi
-Kulaani vitendo vya kigaidi
-Kujaribu kutambua vichochezi vya mashambulizi na kujaribu kuvitatua kwa mashauriano
-Kuwekewa vikwazo kwa mataifa yaliyo na magaidi

4x1 = Alama 4
Utiririko = Alama

## MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

**(a) i.Taja vigezo viwili vya kuanisha irabu. (alama 1)**

mkao wa midomo

sehemu ya ulimi kinywani

**ii. Tofautisha sauti zifuatazo.(alama.2)**

**a. /a/ na /u/**

/a/ ni sauti ya chini kati ilhali /u/ ni sauti ya nyuma juu

/a/ midomo hutandazwa ilhali /u/ midomo huviringwa

**b. /e/ na /o/**

**/e**/ sauti ya mbele kati /o/ sauti ya nyuma kati

**/e/** midomo hutandazwa /o/ midomo huviringwa

**(b) Ainisha aina za vivumishi katika sentensi ifuatayo.(alama. 2)**

**Mwalimu mzee alitufundisha vizuri ile mada ngumu.**

Mzee – kivumishi jina, ile- V kionyeshi/ kiashiria, ngumu- sifa,

**i. i.Eleza maana ya kirai. (alama.1)**

fungu la maneno lisilo na muundo wa kiima kiarifa au kipashio cha kimuundo cha sentensi ambacho hakiwasilishi maana kamilifu.

**ii. Tunga sentensi iliyo na kirai kivumishi na kirai nomino chenye muundo wa W+ V (alama 1)**

Mwanafunzi **<u>yule mwerevu</u>** alisoma **<u>kile kizuri.</u>**

**Kirai kivumishi kirai nomino(W+V)**

**(c) Andika sentensi hii upya bila kubadilisha maana ukitumia "O" rejeshi. (alama 2)**

**Mwanafunzi alitumwa nyumbani juzi na hajapata karo hadi leo.**

Mwanafunzi aliyetumwa nyumbani juzi hajapata karo hadi leo.

**(d) Badilisha sentensi ifuatayo iwe katika hali ya udogo wingi.**

**Kono lake lilivimba baada ya kumwa na jibwa. (alama 2)**

Vijikono vyao vilivimba baada ya kumwa na vijibwa.

**(e) Tunga sentensi iliyo: (alama 3)**

**Kitenzi kishirikishi kikamilifu.**

Mama angali nyumbani.

**Kivumishi kimilikishi nafsi ya pili wingi**

Vitabu vyenu vinahitajika.- mzizi –enu uwepo.

**Kiwakilishi cha nafsi ya tatu tegemezi wingi.**

Wanasoma vitabu vyao. Kiambishi **wa**

**(f) Kanusha sentensi ifuatayo kisha ueleze maana yake katika hali kanushi (alama 2)**

**Angeongoza darasa lake, angepewa tuzo.**

Asingeongoza darasa lake, asingepewa tuzo.

Maana: aliongoza vizuri na akapewa tuzo

**(g) Onyesha sehemu za kisarufi katika neno lifuatalo. (alama 2)**

**Kililiwa**

Ki- ngeli

**l**i- **wakati uliopita**

**l**- mzizi

**iw -** kauli

**a-kiishio**

**(h) Kanusha katika hali timilifu wakati uliopita.**

**Kamati ya uchaguzi iliandaa ripoti kuhusu utovu wa nidhamu shuleni. (alama 2)**

Kamati ya uchaguzi ilikuwa haijandaa ripoti kuhusu utovu wa nidhamu shuleni.

**(i) Changanua kwa kutumia mchoro wa matawi**

**Hatukuondoka na yeye japo tulirudi naye. (alama 4)**

**S1 +U + S2**


**S1---- KN--0**

**KT-----T+H+W**

**U---japo**

**KN--O**

**KT-------T+W**




Mwanafunzi achore mchoro wa matawi

(j) **Tumia kiambishi KA katika sentensi ili kuleta dhana ya: (alama 2)**

i. **Wakati usiodhihirika**

Mwalimu kaondoka.

ii. **Kuonyesha matokeo yanayosababishwa na kitendo.**

Alisoma sana akapita mtihani

**(k) Chane kwa mtama** shumbi**kwa udongo. (alama 1)**

**(l) a. Eleza maana ya fungu tenzi.(alama 1)**

Ni kitenzi kilichoundwa kwa viambishi tofautitofauti.

**b.Taja aina mbili za fungu tenzi. (alama.2)**

fungu tenzi kama sentensi sahili

fungu tenzi kama kishazi tegemezi

**(m) Geuza sentensi hii hadi usemi halisi.**

**Wanakijiji walikuwa wanataka kujua iwapo vipakatalishi vya shule za msingi vingeweza kuinua kiwango cha elimu. (alama 3)**

**"**Vipakatalishi vya shule za msingi vitaweza kuinua kiwango cha elimu?" wanakijiji waliuliza.

**(n) a. Eleza maana ya yambwa. (alama 1)**

yambwa ni nomino tendwa au tendewa

**b. Tunga sentensi iliyo na: shamirisho kipozi na chagizo cha kiasi kamili. (alama.2)**

Mwanafunzi alisoma kitabu **mara tatu.**

Kitabu- kipozi

Mara tatu- chagizo cha kiasi

**(o) Tunga sentensi kwa kutumia kiunganishi cha wakati.(alama 2)**

Mwizi aliwawaiba kondoo halafu akawachinja.

Kisha,baadaye

**(p) Andika visawe vya maneno yaliyopigigwa mstari . (alama 2)**

**Tulienda kusali siku ya Jumapili.**

Kusali- kuomba, kuabudu

Jumapili- dominika

**SWALI LA 4: ISIMU JAMII**

Eleza changamoto zinazokumba ukuaji wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. ( alama 10)

1. Athari za lugha ya kwanza / kigeni.
2. Kinadunishwa – Kiswahili huhusishwa na wasiosoma.
3. Matumizi ya sheng'
4. Ukosefu wa vifaa kama vile vitabu
5. Vyombo vya habari.
6. Ukosefu wa utafiti.
7. Vipindi vichache shuleni.
8. Sera mbovu ya lugha nchini

Ondoa nusu ( ½ ) alama kwa kila kosa la hijai – hadi 4
Ondoa nusu ( ½ ) alama kwa kila kosa la sarufi hadi makosa 4.

(**Hojazozote 5x2**)